TANGAZO LA SERIKALI Na. 266 la tarehe 31/3/2023

SHERIA YA MISITU,

(SURA YA 323)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 106(1)(aa))*

KANUNI ZA USAFIRISHAJI WA MAZAO YA MISITU KUINGIA NDANI YA NCHI NA KUTOKA NJE YA NCHI ZA MWAKA 2023

MPANGILIO WA KANUNI

*Kanun iJina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
UTARATIBU WA USAFIRISHAJI WA MAZAO YA MISITU KUINGIA NDANI YA NCHI

4. Utaratibu wa maombi ya kibali cha kusafirisha mazao ya misitu kuingia ndani ya nchi.
5. Uchakataji wa maombi na kutolewa kwa kibali.
6. Vituo vya ukaguzi wa mazao ya misitu.
7. Ukaguzi wa mazao ya misitu yanayoingia ndani ya nchi.
8. Cheti cha kuingizamazaoyamisitu.

SEHEMU YA TATU
USAFIRISHAJI WA MAZAO YA MISITU NJE YA NCHI

9. Utaratibu wa maombi ya kibali cha kusafirisha mazao ya misitu kwenda nje ya nchi.
10. Uchakataji wa maombi na kutolewa kwa kibali.

11. Ukaguzi na upangaji wa madaraja.
12. Cheti cha kusafirisha mazao ya misitu nje ya nchi.
13. Ukaguzi wa mazao ya misitu yanayosafirishwa kwenda nje ya nchi.

SEHEMU YA NNE
MASHARTI MENGINEYO

14. Kusitishwakwakibali.
15. Taarifaya utekelezaji.
16. Rufaa.
17. Kufutwa.

———

MAJEDWALI

———

SHERIA YA MISITU,

(SURA YA 323)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 106(1)(aa))*

KANUNI ZA USAFIRISHAJI WA MAZAO YA MISITU KUINGIA NDANI YA NCHI NA KUTOKA NJE YA NCHI ZA MWAKA 2023

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1.Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Usafirishaji wa Mazao ya Misitu Kuingia Ndani ya Nchi na Kutoka Nje ya Nchi za Mwaka 2023.

Matumizi

2.Kanuni hizi zitatumika kwa mazao yote ya misitu yanayo safirishwa kuingia ndani ya nchi na kutoka nje y anchi.

Tafsiri

3.Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"afisa leseni" maanayake ni afisaa liyeidhinishwa kutoa leseni chini ya Sheria;

"afisa uhifadhi" maanayakeniafisauhifadhiwaWakalawaHuduma za Misitu Tanzania;

"afisa uhifadhi wa wilaya" maana yake ni afisa uhifadhi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania katika Wilaya husika.

"bidhaa ghafi" maana yake ni bidhaa zilizo chakatwa kiasi;

"hati ya kusafirisha mazao ya misitu nje ya nchi" inamaana iliyotolewa katika Sheria;

Sura ya 323

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Misitu; na

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya misitu.

## SEHEMU YA PILI
## UTARATIBU WA USAFIRISHAJI WA MAZAO YA MISITU KUINGIA NDANI YA NCHI

Utaratibu wa maombi ya kibali cha kusafirisha mazao ya misitu kuingia ndani ya nchi

4.-(1) Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 64 cha Sheria, mtu yeyote anaweza kuingiza mazao ya misitu kutoka nje ya nchi baada ya kupata kibali kutoka kwa Kamishna wa Uhifadhi au afisa leseni aliyekasimishwa mamlaka hayo kwa maandishi na Kamishna wa Uhifadhi.

(2) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), mtu yeyote anayetaka kuingiza mazao ya misitu kutoka nje ya nchi anatakiwa kutimiza masharti yafuatayo:

(a) kuwasilisha maombi kwa afisa uhifadhi wa wilaya husika katika Fomu Na. 1 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi; na

TS Na. 153 la 2004

(b) kulipa ada ya maombi kwa mujibu wa Kanuni za Misitu.

(3) Maombi yaliyowasilishwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) yatatakiwa kuambatana na nyaraka zifuatazo:

(a) kuambatisha nakala ya cheti cha usajili wa biashara ya mazao ya misitu;
(b) leseni ya biashara kwa ajili ya kuingiza ndani ya nchi mazao ya misitu kutoka kwenye mamlaka husika; na
(c) hati safi ya mlipa kodi.

Uchakataji wa maombi na kutolewa kwa kibali

5.-(1) Afisa uhifadhi wa wilaya, baada ya kupokea maombi yaliyoainishwa katika kanuni ya 4, atayachakata na iwapo ataona yamekidhi vigezo atayawasilisha kwa Kamishna wa Uhifadhi ndani ya siku saba tangu tarehe ya kupokea maombi pamoja n mapendekezo yake.

(2) Kamishna wa Uhifadhi, baada ya kupokea maombi na mapendekezo yaliyowasilishwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1), atayafanyiakazi ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya kuyapokea na kutoa uamuzi ambao unaweza kuwa wa-

(a) Kutoa kibali cha kuingiza mazao ya misitu kutoka nje ya nchi katika Fomu Na. 2 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanun ihizi; au
(b) Kukataa kutoa kibali na kuto asababu katika Fomu Na. 3

iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi.

Vituo vya ukaguzi wa mazao ya misitu

6.Kutakuwa na vituo vya ukaguzi wa mazao ya misitu yanayosafirishwa kuingia ndani ya nchi na kutoka nje ya nchi kama vilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Kanuni hizi.

Ukaguzi wa mazao ya misitu yanayoingia ndani ya nchi

7.-(1) Mtu yeyote aliyepata kibali cha kuingiza mazao ya misitu ndani ya nchi kwa mujibu wa Kanuni hizi atatakiwa kukaguliwa na afisa ukaguzi wa kituo cha ukaguzi wa mazao ya misitu vilivyoanishwa katika Kanuni hizi.

(2)Afisaukaguziwakituohusikaatatakiwakujiridhishakuwepokwa nyarakazifuatazaokablayakuruhusumazaoyamisitukuingiandaniyanchi:

(a) kibali cha kuingizamazaoyamisitundaniyanchikwamujibuwaKanunihizi;
(b) kibali cha kusafirishamazaokutokanchihusika;
(c) cheti cha uasiliwamazao; na
(d) cheti cha usafiwamimeakilichotolewananchihusika.

Cheti cha kuingiza mazao ya misitu

8. Baada ya afisa ukaguzi kukamilisha ukaguzi na kujiridhisha kuwa masharti yaliyo ainishwa katika kanuni ya 7 yamezingatiwa, afisa leseni wa eneohusika atatoa cheti cha kuingiza mazao ya misitu ndani ya nchi katika Fomu Na. 4 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi.

## SEHEMU YA TATU
## UTARATIBU WA USAFIRISHAJI WA MAZAO YA MISITU KWENDA NJE YA NCHI

Utaratibu wa maombi ya kibali cha kusafirisha mazao ya misitu kwenda nje ya nchi

9.-(1) Mtu yeyote anaweza kusafirisha mazao ya misitu kwenda nje ya nchi baada ya kupata kibali kutoka kwa Kamishna wa Uhifadhi au afisa leseni aliyekasimishwa mamlaka hayo kwa maandishi na Kamishna wa Uhifadhi.

(2) Masharti ya kanuni ndogo ya (1) hayatatumika kwa-

(a) misandali, isipokuwa kwa mazao ya miti ya misandali yaliyo ingizwa kutoka nje ya nchi na kuchakatwa nchini; na

(b) mpingo, isipokuwa bidhaa ghafi zinazotokana na mazao ya mitihiyo.

(3) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), mtu yeyote anayetaka kusafirisha mazao ya misitu kwendanje ya nchi anatakiwa kutimiza masharti yafuatayo-

(a) kuwasilisha maombi, katika Fomu Na. 5 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi, kwa afisa uhifadhi wa wilaya ambayo uvunaji wa mazao ya misitu husika umefanyika; na

TS Na. 153 la 2004

(b) kulipa ada ya maombi kwa mujibu wa Kanuni za Misitu.

(4) Fomu ya maombi itakayowasilishwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (2) inatakiwa kuambatana na nyaraka zifuatazo-

(a) cheti cha usajili wa kampuni au cheti cha usajili wa jina la biashara;

(b) Namba ya Utambulisho ya Mlipa Kodi;

(c) cheti cha usajili wa kodi ya Ongezeko la Thamani;

(d) cheti cha usajili wa biashara ya mazao ya misitu;

(e) cheti cha mgao wa uvunaji kwa mazao ya misitu kutoka miti ya asili;

(f) leseni ya uvunaji wa mazao ya misitukwa mazao ya misitu ya miti ya asili;

(g) kibali cha kusafirisha mazao ya misitu kutoka eneo la uvunaji kwenda kwenye ghala au kiwanda cha kupasuliambao au kutoka kiwanda cha kupasulia mbao kwenda kwenye ghala;

(h) leseni ya biashara kwa ajili ya kusafirisha mazao ya misitu kwenda nje ya nchi kutoka kwenye mamlaka husika;

(i) cheti safi cha mlipakodi;

(j) dhamana ya muamala wa ahadi inayotolewa na benki kwenda benki nyingine ilikuthibitisha malipo yatafanyika au mkataba wa biashara na oda iliyothibitishwa kutoka kwa mnunuzi;

(k) uthibitisho wa kuwa n aakaunti ya fedha za kigeni; na

(l) taarifa za mapato ya fedha za kigeni iliyothibitishwa na benki anayotumia kwenye biashara yake isipokuwa kwamba, sharti hili halitawahusu wafanya biashara wanaosafirisha mazao ya misitu kwa maraya kwanza.

Uchakataji wa maombi na

10.-(1) Afisa uhifadhi wa wilaya, baada ya kupokea maombi yaliyoainishwa katika kanuni ya (9), atayachakata na iwapoatao na yamekidhi vigezo atayawasilisha kwa Kamishna wa Uhifadhi ndani ya

kutolewa kwa kibali

siku saba tangu tarehe ya kupokea maombi pamoja na mapendekezo yake.

(2) Kamishna wa Uhifadhi, baada ya kupokea maombi na mapendekezo yaliyowasilishwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1), atayafanyia kazi ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya kuyapokea na kutoa uamuzi ambao unaweza kuwa wa-

(a) kutoa kibali cha kusafirisha mazao ya misitu kwenda nje ya nchi katika Fomu Na. 6 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi; au

(b) kukataa kutoa kibali na kutoa sababu katika Fomu Na. 7 iliyoainishwa katika Jedwali la Kanuni hizi.

Ukaguzi na upangaji wa madaraja

11.-(1) Mtu yeyote atakayepata kibali cha kusafirisha mazao ya misitu kwenda nje ya nchi kwa mujibu wa kanuni ya 10 atawasilisha maombi ya ukaguzi na kupangiwa daraja kwa afisa uhifadhi wa wilaya katika Fomu Na. 8 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi.

(2) Maombi yatakayowasilishwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) yatatakiwa kuambatana na kibali cha kusafirisha mazao ya misitu nje ya nchi kilichotolewa kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(3) Baada ya kupokea maombi hayo, afisa uhifadhi wa wilaya atafanyaukaguzi na kupanga madaraja katika ghala la mwombaji lililobainishwa katika cheti cha usajili wa biashara ya mazao y amisitu au kiwanda cha kupasuliambao kilichosajiliwa kwa mujibu wa Sheria.

(4) Baada ya kufanya ukaguzi na kupanga madaraja kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (3), afisa uhifadhi wa wilaya atatoa cheti cha ukaguzi na cheti cha madaraja kwa mwombaji katika Fomu Na. 9 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi.

Cheti cha kusafirisha mazao ya misitu nje ya nchi

12.-(1) Mtu yeyote anayetaka kusafirisha mazao ya misitu nje ya nchi na aliyekaguliwa na kupangiwa madaraja ya mazao husika kwa mujibu wa kanuni ya 11, atatakiwa kuwasilisha maombi ya kupatiwa cheti cha kusafirisha mazao ya misitu nje ya nchi kwa afisa uhifadhi wa wilaya ambayo uvunaji wa mazao ya misitu husika umefanyika.

(2) Maombi chini ya kanuni ndogo ya (1) yatakuwa katika Fomu Na. 10 iliyoainishwakatikaJedwali la Kwanza la Kanuni hizi na yataambatana na kibali cha kusafirisha mazao ya misitu kwenda nje ya nchi, cheti cha ukaguzi na cheti cha madaraja ya mazao husuka vilivyotolewa kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(3) Afisa uhifadhi wa wilaya, baada ya kupokea maombi yaliyowasilishwa chini ya kanuni ndogo ya (2), atayawasilisha kwa Kamishna wa Uhifadhi ndani ya siku saba tangu tarehe ya kupokea

maombi hayo pamoja na mapendekezo yake.

(4) Kamishna wa Uhifadhi, baada ya kupokea maombi na mapendekezo yaliyowasilishwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1), atayafanyiakazi ndani ya siku saba tangu tarehe ya kuyapokea na kutoa uamuzi ambao unaweza kuwa wa-

(a) kutoa cheti cha kusafirisha mazao ya misitu kwenda nje ya nchi katika Fomu Na. 11 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi; au

(b) kukataa kutoa cheti na kutoa sababu.

Ukaguzi wa mazao ya misitu yanayosafirishwa kwenda nje ya nchi

13.-(1) Mtu yeyote aliyepata kibali na cheti cha kusafirisha mazao ya misitu kwenda nje ya nchi kwa mujibu wa Kanuni hizi atatakiwa kukaguliwa na afisa mkaguzi wa kituo cha ukaguziwamazaoyamisituvilioanishwakatikaKanunihizi.

(2) Afisa ukaguzi wa kituo husika atatakiwa kujiridhisha kuwepo kwa nyaraka zifuatazo kabla ya kuruhusu mazao ya misitu kusafirishwa kwenda nje ya nchi:

(a) kibali cha kusafirisha mazao ya misitu kwenda nje ya nchi kwa mujibu wa Kanuni hizi;

(b) cheti cha ukaguzi;

(c) cheti cha madaraja; na

(d) cheti cha kusafirisha mazao ya misitu kwenda nje ya nchi kwa mujibu wa Kanuni hizi.

SEHEMU YA NNE
MASHARTI MENGINEYO

Kusitishwa kwa kibali

14.Kamishna wa Uhifadhi anaweza kusitisha kibali chochote kilichotolewa kwa mujibu wa kanuni hizi endapo-

(a) itabainika kuwa mwenye kibali amekipata kwa njia ya udanganyifu; au

(b) mwenye kibali amekiuka masharti yoyote ya Sheria au Kanuni hizi.

Taarifa ya utekelezaji

15. Kamishna wa Uhifadhi atawasilisha kwa Waziri taarifa ya utekelezaji kila baada ya miezi mitatu kuhusiana na:

(a) idadi ya vibali vyote vilivyotolewa kwa mujibu wa Kanuni hizi, na

(b) idadi ya vibali vilivyokataliwa na sababu za

kukataliwa.

Rufaa

16. Mtu yeyote ambaye hataridhika na uamuzi wowote uliofanywa chini ya Kanuni hizi anaweza kukatarufaa kwa Waziri ndani ya siku thelathini kuanzia tarehe uamuzi ulipotolewa.

Kufut wa TS. Na. 181 la 2007; na 334 la 2004

17. Kanuni zifuatazo zinafutwa:

(a) Kanuni za Kuingiza Mazao ya Misitu Nchini za Mwaka 2007; na

(b) Kanuni za Katazo la Kusafirisha Nje ya Nchi Miti Laini na Miti Migumu katika Mfumo wa Mizizi, Fito na Nguzo za Mwaka 2004.

JEDWALI LA KWANZA

(*Limetengenezwa chini ya kifungu cha 4(2),5(2),8, 9(3), 10(2), 11,12(2) na 12(4))*

FOMU

FOMU NA. 1

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 4(2))*

MAOMBI YA KIBALI CHA KUINGIZA MAZAO YA MISITU NCHINI

Mimi/Sisi mwenye saini yangu hapa chini naomba kibali cha kuingiza mazao yafuatayo ndani ya nchi

| NA. | MAZAO YA MISITU | AINA YA MITI (SPISHI) | VIPIMO | UJAZO/TANI/CBM/ VIPANDE |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

1. Jina (Kampuni au mtu binafsi) ………………………………………………….
2. Anwani …………………………… na namba ya simu ………………………….
3. Jina la nchi na eneo mazao yanapotoka …………………………………………
4. Kituo mazao yatakapoingilia nchini …………………………………………….

Tarehe……………………… Saini yaMwombaji ………………………………….

FOMU NA. 2

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 5(2)(a))*

KIBALI CHA KUINGIZA MAZAO YA MISITU NDANI YA NCHI

Kibali kinatolewa kwa ………………………………… wa ……………………
Kuingiza nchini kupitia bandari/ kituo cha ………………………………………………

Mazao ya misitu yanaingizwa kutoka Nchi ya …………………………….. ………….
Mazao yanayoingizwa nchini:

1. Mazao ya Misitu ………………………
2. Aina (Spishi) ……………………..
3. Ujazo (TANI/CBM) ………………..
4. Vipimo …………………….
5. Idadi ya vipande: ………….
6. Sehemu zao lilipotolewa: ………………….

Jina …………………………
Cheo ………………………..
Saini ………………………

Tarehe……………………………….. Muhuri ……………………………

FOMU NA. 3

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 5(2)(b))*

TAARIFA YA KUKATALIWA KWA KIBALI CHA KUINGIZA MAZAO YA MISITU NCHINI

Kwa: ……………………………………………….
*(Mwombaji)*
Anwani …………………………………..
……………………………………………….
……………………………………………….
……………………………………………….

Unajulishwa kuwa maombi yako ya kupatiwa kibali cha kuingiza mazao ya misitu nchini kutoka ………………………………..yamekataliwa kwa sababu zifuatazo ………………………………………………………………………………………………… ……………………………………………………………………………

Kituo ……………………………………………………………

Jina na Saini ya Afisa Uhifadhi wa Wilaya …………………………….

Tarehe ……………………………………..Muhuri………………………..

FOMU NA. 4

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 8)*

CHETI CHA KUINGIZA MAZAO YA MISITU NDANI YA NCHI

Cheti hiki kimetolewa kwa ………………………………………………………………. Wilaya ya ………..………………………….. cha kuingiza mazao ya misitu aina ya ………………………………. kutoka …………………… …………………. Mazao hayo yamekaguliwa na kuthibitishwa kuwa yamezingatia vigezo na masharti vilivyo ainishwa katika Kanuni hizi.

UTHIBITISHO

Mimi…………………………………………………… Kamishna wa Uhifadhi, nathibitisha kuwa mazao yanayoingizwa ndani ya nchi yamezingatia vigezo na masharti vilivyoainishwa katika Kanuni hizi.

Jina ……………………………………
Saini ………………………………… ………………..
Kamishna wa Uhifadhi Tarehe

FOMU NA. 5

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 9(3)(a))*

MAOMBI YA KIBALI CHA USAFIRISHAJI WA MAZAO YA MISITU NJE YA NCHI

Mimi/Sisi mwenye saini yangu hapa chini naomba kibali cha kusafirisha mazao yafuatayo kwenda nje ya Nchi

| NA. | MAZAO YA MISITU | AINA/SPISHI | VIPIMO | UJAZO/TANI/CBM/ VIPANDE |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

1. Jina (Kampuni au mtu binafsi)…………………………………………
2. Anwani…………………………………Namba ya simu…………………..
3. Jina na anuani ya benki anayotumia muombaji yenye akaunti ya fedha za kigeni……………………………………………………………
4. Nchi ambako mazao ya misitu yanaelekea…………………….……….. ……………………………………………………………...…………..
5. Sehemu yanayopitia kwenda nje ya nchi ………………………………
6. Tarehe ya kusafirisha………………………………………………..
7. Kituo cha kupokelea mazao hayo………………………………………

Jina la Mwombaji …………………………….

Saini …………………………………

Tarehe……………………………….

B: KWA MATUMIZI YA OFISI TU

Mimi …………………………………………....Cheo ……..……………… Napendekeza Ndugu / Kampuni ……………………………………… wa (Anwani)…………………………..apewe / Asipewe kibali cha kusafirisha nje ya nchi mazao ya Misitu yaliyoorodheshwa hapo juu kwa sababu zifuatazo:
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

Saini ……………………………………… Wilaya ………………………………..Tarehe………………………………….

FOMU NA. 6

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 10(2)(a))*

KIBALI CHA USAFIRISHAJI WA MAZAO YA MISITU NJE YA NCHI

Ruhusa imetolewa kwa …………………………………………..wa……………………………………………
Kusafirisha mazao ya misitu kupitia bandari/kiwanja cha ndege/kituo cha………………………………………………………….
Bidhaa/Mazao yanayosafirishwa yanaelekea kwa (Anwani)……….………………………………………………..
Nchi………………………………………………

1. Mazao/bidhaa zinazosafirishwa…………………………………………….
2. Spishi/Aina……………………………..
3. Ujazo/uzito…………………………….
4. Idadi…………………………………
5. Mwisho wa matumizi wa kibalihiki……………………………………..
6. Saini…………………………………….
7. Tarehe ya kutolewa kibali ……………………

UTHIBITISHO

Mimi………………………….………..Kamishna wa Uhifadhi, nathibitisha kuwa mazao yaliyoidhinishwa kusafirishwa nje ya nchi, yamevunwa katika msitu unaosimamiwa Tanzania.

Jina……………………………

Saini……………………….. …………..…………..

Kamishna wa Uhifadhi Tarehe

FOMU NA. 7

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 10(2)(b))*

TAARIFA YA KUKATALIWA KWA KIBALI CHA KUSAFIRISHA MAZAO YA MISITU NJE YA NCHI

Kwa: ……………………………………………….
(Mwombaji)
Anwani …………………………………..
……………………………………………….
……………………………………………….
……………………………………………….

Unajulishwa kuwa maombi yako ya kupatiwa hati kusafirisha mazao ya misitu kuelekea ………..yamekataliwa kwa sababu zifuatazo……………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………

Kituo ………………………………………………
JINA NA SAINI ya Afisa Mhifadhi wa Wilaya ……………………………………….

TAREHE……………………………………..MUHURI………………………..

FOMU NA. 8

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 11(1))*

MAOMBI YAUKAGUZI NA KUPANGIWA DARAJA

Mimi/Sisi mwenye saini yangu hapa chini naomba kufanyiwa ukaguzi na kupangiwa daraja la mazao ya misitu.

| NA. | MAZAO YA MISITU | AINA YA MITI (SPISHI) | VIPIMO | UJAZO/TANI/CBM/ VIPANDE |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

1. Jina (Kampuni au mtubinafsi…………………………………………………….
2. Anwani……………………………na namba ya simu………………………….
3. Eneo ambalo Ghala lipo …………………………………………

Tarehe……………………Saini ya Mwombaji ………………………………….

FOMU NA. 9

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 11(4))*

CHETI CHA UKAGUZI NA KUPANGIWA DARAJA

Mimi ………………………………………………………………. Nathibitisha kuwa nimekagua na kupanga daraja la mazao ya misitu yanayomilikiwa na ………………………………………………………………………………………… yaliyopo ………………………………………………………… na kubaini kuwa yamekidhi masharti ya Kanuni za Misitu Tangazo la Serikali Na. 153 la Mwaka 2004 na Sheria ya Misitu ya Mwaka 2002.

Cheti hiki kimetolewa bila marekebisho au mabadiliko yoyote.

Leo tarehe………………………………..Mwezi…………………….. 20 ………………

................................
Saini ya Afisa Mkaguzi

FOMU NA. 10

*(Imetengenezwa chini ya kanui ya 12(2))*

MAOMBI YA CHETI CHA KUSAFIRISHA MAZAO YA MISITU NJE YA NCHI

Mimi/Sisi mwenye saini yangu hap achini na omba Cheti cha kusafirisha mazao yafuatayo nje ya nchi

| NA. | AINA YA MAZAO YA MISITU | DARAJA NA ALAMA YA DARAJA | ALAMA YA UTAMBUZI WA MAZAO YA MISITU | UJAZO/TANI/CBM / VIPANDE |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

Mimi ……………………………………………. Cheo …………………………………………………… Napendekeza Ndugu / Kampuni …………………………………… wa (Anwani)…………………………..apewe / Asipewe kibali cha kusafirisha nje ya nchi mazao ya Misitu yaliyoorodheshwa hapo juu kwa sababu zifuatazo:
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

Saini …………………………………… Wilaya ………………………………..Tarehe………………………………….

FOMU NA. 11

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 12(4)(a))*

CHETI CHA KUSAFIRISHA MAZAO YA MISITU NJE YA NCHI

Cheti hiki kimetolewa kwa ………………………………………………………………. Wilaya ya ………..………………………….. cha kusafirishamazaoyamisituainaya ………………………………….kutoka bandari ya ……………………… ……….
Mazao ya misitu yaliyoainishwa ujazo wa ………………………… yat asafirishwa kwenda……………………………….

Mazao hayo yamepewa daraja na kuwekwa alama kama ilivyoonyeshwa.

(1) Aina za MazaoyaMisitu
(2) UasiliwaGhala
(3) Alama zilizowekwa kwa ajili ya kusafirisha
(4) Idadi ya vipande
(5) Uhalali
(6) Saini ya Kamishna wa Uhifadhi
(7) Sehemu kilipotolewa
(8) Tarehe
(9) Maoni

UTHIBITISHO

Mimi…………………………………………………… .Kamishna wa Uhifadhi, nathibitisha kuwa mazao yaliyoidhinishwa kusafirishwa nje ya nchi, yamevunwa katika msitu unaosimamiwa Tanzania.

Jina……………………………………

Saini……………………………………  ……………………....

Kamishna wa Uhifadhi  Tarehe

*Tangazo la Serikali Na. 266 (Linaendelea.)*

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 6)*

VITUO VYA KUINGIA NA KUTOKA NCHINI

Vituo vya kuingia/ kutoka Nchini

(a) Barabara:
- Holili (Rombo)
- Namanga (Arusha)
- Sirari (Tarime)
- Mutukula (Kagera)
- Tunduma (Momba)
- Namkale (Rukwa)
- Kasumulu (Kyela)
- Kyaka (Kagera)
- Horohoro (Mkinga)
- Tarekea (Rombo)
- Rusahunga (Biharamulo)
- Mtambaswala (Nanyumbu)
- Newala (Chihanga)
- Tunduru (Makande)
- Kabanga (Ngara)
- Rusumo (Ngara)

(b) Reli:
- Moshi
- Arusha
- Tunduma
- Kahe junction

(c) Bandari
- Dar es Salaam (Bahariya Hindi)
- Lindi (Bahariya Hindi)
- Mtwara (Bahariya Hindi)
- Mafia (Bahariya Hindi)
- Kilwamasoko (Bahariya Hindi)
- Bagamoyo (Bahariya Hindi)
- Pangani (Bahariya Hindi)
- Tanga (Bahariya Hindi)
- Mbwera (Bahariya Hindi)
- Kasanga (Ziwa Tanganyika)
- Kibirizi (Ziwa Tanganyika)
- Kigoma (Ziwa Tanganyika)

Dodoma,
23 Machi, 2023

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Maliasili na Utalii*